

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO: DOMINIKA 28 YA MWAKA C - 12.10.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 12.10.2025 | **DOMINIKA YA 28 YA MWAKA C WA KANISA**<br><br>Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi. |
| 2. | JUMANNE 14.10.2025 | **Nyerere Day** – siku ya mapumziko<br>UWAKA wote na familia kusali pamoja na kutegemeza Masista Dada Wadogo Visiga. Mchango wa usafiri shs. 10,000/= kwa kila mshiriki. Mchango unapokelewa na Mtunzahazina wa UWAKA Parokia. |
| 3. | JUMATANO 15.10.2025 | Kumbukumbu ya Mt. Theresa wa Avila, Mwalimu wa Kanisa<br>Kumbukumbu ya Kutabarukiwa Kanisa Kuu la Jimbo, Mt. Yosefu |
| 4. | JUMAMOSI 18.10.2025 | **Sikukuu ya Mt. Luka Mwinjili.** Kutakuwa na Misa katika Kanda C kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria na kukabidhi **Kanda D na E**, **saa 1:00 asubuhi.** |
| 5. | JUMAMOSI 18.10.2025 | Misa ya kilele ya Jubilei ya Miaka 200 ya kuzaliwa kwa Kardinali Charles Lavigerie, mwanzilishi wa Shirika la Mapadre Wamisionari wa Afrika (MAfr.) na Shirika la Masista wa Mama Yetu wa Afrika (MSOLA). Misa itaadhimishwa hapa Parokiani na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Sana Judde Thaddaeus Ruwa'ichi OFMCap. kuanzia saa 3:00 asubuhi. Sisi wenyeji, tufike saa 2:00 asubuhi kumpokea Askofu Mkuu. Baada ya Misa tutakuwa na tafrija kwa uwakilishi wa kijumuiya na kivyama kwa njia ya kuponi. |
| 6. | DOMINIKA 19.10.2025<br><br>DOMINIKA YA UMISIONARI | **DOMINIKA YA 29 YA MWAKA C**<br><br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Gregory VII<br>Watangaza Neno: Yuda Thadei na Oresta Luambano<br><br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Maximilian Kolbe<br>Watangaza Neno: Timothy Mwidete na Angela Komba<br><br>**Misa ya 3: Saa 5:00 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Gregory VII na Mt. Maximilian Kolbe<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya Uenezaji wa Injili (Misioni). |
| 7. | MABINTI WA MARIA MKINGIWA | Shirika la Mabinti wa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili wana ujumbe kwetu wazazi; tuwaruhusu mabinti wawe wafuasi wa Mama |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | ROZARI KUOMBEA AMANI DUNIANI | Jumamosi ijayo ni siku maalum kwa Utoto Mtakatifu kusali Rozari kuombea Amani duniani. Hapa Parokiani watoto wataanza kusali saa 2:30 asubuhi ili kupisha Misa ya Jubilei saa 3:00 asubuhi. |
| 9. | USAFI WA KANISA | Kutokana na maandalizi ya Misa ya Jubilei Jumamosi, Jumuiya za zamu na wote wenye mapenzi mema wanaalikwa kwa usafi **Ijumaa saa 2:00 asubuhi.** |
| 10. | VITI VYA PAROKIA | Parokia ipo mbioni kununua viti vipya. Hivyo viti vinavyotumika sasa ukumbini vitauzwa kwa Jumuiya zinazohitaji kwa kati y ash. 5,000 na 10,000/= kwa kiti kuanzia leo saa 5:00 asubuhi. |
| 11. | MAFUNDISHO YA KOMUNYO NA KIPAIMARA | Mafundisho yameanza rasmi jana. Ili kuweka uelewa wa pamoja tangu mwanzo, kutakuwa na kikao cha wazazi na walezi wa Watoto wa Kipaimara na Komunio Dominika ijayo baada ya Misa ya kwanza. Jumamosi ijayo hakutakuwa na mafundisho kutokana na Misa ya Jubilei ya Kardinali Lavigerie. |
| 12. | RATIBA YA MAVUNO PAROKIA 2025 | Baada ya uzinduzi wa Mavuno Parokia Dominika iliyopita, viongozi wa Jumuiya wanatakiwa kufuatilia familia ambazo bado kuahidi na walioahidi kuanza kukamilisha na mwisho ni siku ya kilele 02.11.2025 tutakapopokea na kufanya mnada wa mavuno ya vitu. |
| 13. | UCHAGUZI WA VIONGOZI WA VYAMA KANDA | Jana ilikuwa siku ya uchaguzi wa UWAKA na WAWATA ngazi ya Kanda. Ambao hawakuweza kufanya wapange utaritabu kukamilisha. Wazee na VIWAWA uchaguzi utafanyika 25.10.2025. |
| 14. | UTUME WA FORMER SEMINARIANS JIMBO KUU | Wale wote waliosoma seminari zamani (Former Seminarians) wanaombwa kukutana na Mjumbe toka Jimboni leo mara baada ya Misa ya 1 na ya 2. Lengo ni kuendelea na utume wa Former Seminarians alioanzisha Askofu Mkuu kwa wote waliowahi kupitia Seminari; na kuuendeleza zaidi utume huo katika ngazi ya Parokia. |
| 15. | ELIMU YA USALAMA BARABARANI | Tunawapongeza walioweza kushiriki mafunzo ya Usalama barabarani - kuhusu sheria za barabara na namna ya kuendesha ili kuepuka ajali za barabarani wiki iliyopita, na shukrani kwa waendesha mafunzo. |
| 16. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa 2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>Ada ya ushiriki ni 5,000/=.<br>***Leo kila Jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uandikishaji washiriki wa Warsha kwani inatakiwa Jimboni.*** |
| 17. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini Letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

**MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA ROZARI NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA 2025**

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J |
| 9 | 22/11 – 29/11 | K |

## MATANGAZO NDOA KWA MARA YA TATU

Remigi Reginald Mrema BIN Reginald Ndetola Mrema na Mariana Mtauli Massawe wa Mbezi Mshikamano

Anatarajia kufunga ndoa na:

Lydia Thomas Komu BINTI Thomas Gervas Komu na Rose Daudi Manyanga wa Parokia ya Bikira Maria Madale

**MATANGAZO YA DARAJA YA USHEMASI KWA MARA YA TATU**

Mhashamu Sana Askofu Mkuu, Jude Thaddaeus Ruwa'ichi OFMCap, wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anatangaza Daraja ya Ushemasi kwa Mafrateri wafuatao:

1. Frateri wa Shirika la Ndugu Wadogo Wakapuchini, Frt. William Mohammed Kimaro, Baba: Paskal Mtana na Mama: Phelimedia Uforo Shayo kutoka Parokia ya Mwanagati, Jimbo Kuu la Dar. Anatarajiwa kupewa Ushemasi 17.10.2025 katika Kanisa la Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan Morogoro.

2. Frateri wa Shirika la Misioni: Mapadri wa Mt. Vincent wa Paulo (Vincentian Fathers – CM), Frt. Godfrey Linus Gangisa, Baba: Linus Haule Gangisa na Mama: Agnes C. Mapunda kutoka Parokia ya Epifania Kijichi, Jimbo Kuu la Dar. Anatarajiwa kupewa Ushemasi 01.11.2025 katika Kanisa la Mungu Mwokozi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan Morogoro.

Tuwaombee waweze kufikia Daraja hiyo wanayoitamani

**MASOMO DOMINIKA YA 29 YA MWAKA C – 19.10.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Kut 5:14-17 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 121: 1-8 |
| SOMO II | 2Tim 3:14 – 4:2 |
| SHANGILIO | Yn 17:17 |
| INJILI | Lk 18:1-8 |